- **Katika ngazi ya Wilaya: Wakaguzi wa Shule, Maafisa Elimu, Wahandisi wa Ujenzi na Maafisa Afya** wana wajibu mkubwa wa kuthibitisha kuwa maandalizi ya kutosha kuhusu majengo na mazingira ya Shule kiafya yanafaa kwa matumizi ya Shule. Taarifa zinazoandaliwa na watendaji hao husaidia kutoa picha halisi ya matayarisho na kutoa mapendekezo sahihi pale wanapopitisha fomu za maombi ya kumiliki na kuendesha Shule. Maombi haya husaidia Wizara kupata picha halisi kuhusu matayarisho ya mwombaji na kufanya uamuzi sahihi.
- **Watendaji wa Serikali ya Kijiji/Mitaa na Kata** hutoa taarifa mahususi zinazosaidia kutoa picha ya mahitaji ya Elimu katika eneo lao na kumthibitisha anayetaka kuanzisha Shule kama ndiye mmiliki halali wa eneo la Shule itakapojengwa.
- **Mkaguzi Mkuu wa Shule wa Kanda:** Hufanya ukaguzi maalumu kwa lengo la kusajili shule na hukamilisha fomu Na. RS.8 kisha kutuma fomu hizo kwa Kamishna wa Elimu pamoja na taarifa ya Ukaguzi wa Shule husika. Mkaguzi Mkuu wa Shule husimamia na kutathmini utekelezaji wa mitaala pamoja na uendeshaji wa Shule kwa ujumla.
- **Katibu Tawala wa Mkoa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya.**Husimamia masuala yote ya maendeleo ya Elimu katika maeneo yao. Wana jukumu la kutoa maamuzi juu ya aina ya mipango inayotakiwa kufanywa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Shule za Serikali za Msingi na za Sekondari za kutwa. Wanasimamia uhamasishaji wa maendeleo ya sekta ya Elimu ya jamii inayowazunguka pia wanapokea na kupendekeza maombi ya kutaka kumiliki, kuendesha na kusajili Shule
- **Waziri wa Elimu**, Waziri wa Elimu huthibitisha mwenye Shule na huidhinisha usajili wa Shule za dini.

III. USAJILI WA WALIMU

Usajili wa Walimu unafanywa kwa mujibu wa Sheria namba 25 ya mwaka 1978 sehemu ya VI na rekebisho lake Na. 10 la mwaka 1995 pamoja na kanuni za Elimu za mwaka 2002.

Makundi matatu ya Walimu yanayoweza kusajiliwa.

- Mwalimu aliyefuzu na kufaulu mitihani kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Mtu asiye na taaluma ya Ualimu atakayeomba leseni ya kufundisha.
- Walimu wasio raia wa Tanzania waliofuzu taaluma ya ualimu wanaoomba na kupatiwa leseni ya kufundisha.

Walimu wenye sifa

- Mwalimu mwenye sifa husaini mkataba na mwajiri wake kwa mujibu wa Kanuni za utumishi za Walimu za mwaka 2003 Mwalimu huyu husajiliwa katika rejesta Na. II kama Mwalimu anayesubiri kuthibitishwa.
- Baada ya kumaliza muda wa kusubiri kuthibitishwa wa mwaka mmoja, Mwalimu husajiliwa kwenye rejesta Na. I ya Walimu waliothibitishwa kazini.

Walimu walio na taaluma ya ualimu ambao sio Watanzania wanaotaka kufundisha nchini.

- Mwombaji ataomba kupatiwa leseni ya kufundishia kupitia kwa uongozi wa Shule anayotaka kufundisha na kuyapitisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Shule wa Kanda. Mwombaji anaambatisha vyeti vya taaaluma na umri wake.
- Mkaguzi mkuu wa Shule wa Kanda kupitia na kutoa mapendekezo ya maombi hayo kwa Kamishna wa Elimu.
- Maombi ya ajira ya Ualimu huchambuliwa na kamati maalumu ambayo mwenyekiti wake ni Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala kisha kumshauri Waziri kupitisha maombi hayo.
- Waziri akiridhika hutoa kibali cha kufundisha nchini.
- Kamishna wa Elimu hutoa idhini ya mwombaji kupatiwa leseni.
- Walimu wenye leseni wanasajiliwa kwenye rejesta Na III.

Muhtasari:
Mwongozo wa Usajili wa Shule wa Mwaka 1982 unapatikana katika ofisi za Elimu za Wilaya, Mkoa na Makao Makuu ya Wizara.
Mwongozo huu unatoa tafsiri ya Sheria ya Elimu na kanuni za Elimu kuhusu usajili wa shule na walimu.

Mambo muhimu yaliyopo katika mwongozo ni pamoja na fomu za usajili wa Shule na Walimu. Aina ya fomu (majina mapya katika mabano) hizo ni:

Fomu Na. 6 (RS 6) kuhusu maombi ya kutaka kuwa mwenye Shule na ***fomu Na 7 (RS.7)*** kuhusu maombi ya kutaka kuwa Meneja wa Shule.

Fomu 8 (RS.8) kuhusu maombi ya usajili wa Shule zisizo za Serikali na ***Fomu Na. (RS.9)*** kuhusu maombi ya leseni na usajili wa Shule/ Taasisi za Dini.

Fomu Na. 9 (RS.9) kuhusu maombi ya leseni na usajili wa Shule/ Taasisi za Dini.

Fomu Na. 4 (RT.4) kuhusu maombi ya kutaka kupatiwa leseni ya kufundisha.

Fomu Na. 3 (RS 3) kuhusu taarifa ya kusajiliwa Walimu wenye leseni katika rejesta Na. III..

Fomu Na. 1 (RT.1) kuhusu cheti na taarifa ya kusajiliwa walimu ambao wamemaliza muda wa mwaka 1 wa kusubiri na kuthibitishwa kazini.

Kwa taarifa zaidi wasiliana na mojawapo ya mamlaka zifuatazo: Ofisi za Elimu za Wilaya, Mkoa, Kanda au Makao Makuu ya

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZNAIA

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Mambo muhimu katika Utaratibu wa Usajili wa Shule na Walimu

Sajili Shule Yako sasa
Uchangie Ubora wa Elimu

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi,
S.L.P. 9121, Dar es Salaama - Tanzania.
Simu: +255-22-2120417/+255 22 2120403,
Nukushi: +255-22-2113271,
Teleksi: +255-22-242741 Elimu Tz
Barua Pepe: aek@moec.go.tz

I. UTANGULIZI

Uanzishaji na usajili wa Shule na Walimu ni mojawapo ya majukumu yanayofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuhakikisha kuwa Elimu inayotolewa kwa wadau inazingatia sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisho lake Na. 10 la mwaka 1995.

Maana ya Shule

Shule ni kusanyiko, taasisi, Jumuiya au mahali kwa vyovyote patakavyoitwa, ambapo inatolewa elimu ya awali, msingi, sekondari, elimu ya ualimu au elimu ya watu wazima kwa watu saba au zaidi kwa wakati mmoja, au vinginevyo na ikiwa mafunzo hayo yanatolewa moja kwa moja au kwa njia ya Posta., basi itamaanisha mahali ambapo mafunzo yanatayarishwa au mahali ambapo kazi za wanafunzi zinapokelewa, zinatumwa au zinasahihishwa.

Aina za Shule na Maana zake

"Shule ya Awali" ni shule inayotoa elimu ya awali lakini endapo inatoa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari au Elimu ya Ualimu, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu. Shule ya awali itamaanisha kuwa ni ile inayotoa Elimu ya Awali.

"Shule ya Msingi" ni shule inayotoa elimu lakini endapo shule inatoa Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari kwa mujibu wa Sheria ya Elimu, Shule ya Msingi ni sehemu ya shule kutoa Elimu ya Msingi.

"Shule ya Sekondari" ni Shule inayotoa Elimu ya Sekondari lakini endapo Shule inatoa Elimu ya Sekondari, Msingi, awali na/au Elimu ya Ualimu, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu, Shule ya Sekondari ni ile inayotoa Elimu ya Sekondari.

"Taasisi ya Dini" ni Taasisi yoyote inayoendeshwa na jumuiya ya kidini kwa makusudi ya kuwaandaa watumishi wa dini husika inayoendeshwa baada ya kupatiwa leseni na waziri.

Shule ya mafunzo ya dini (Seminari)" ni mkusanyiko wowote, taasisi, jumuiya au mahali ambapo waziri ameridhika kuwa madhumuni yake au lengo kuu ni kutoa mafunzo ya dini.

Uendeshaji wa Shule

"Meneja" katika mtazamo wa shule ni mtu anayehusika na uendeshaji wa shule au anayesimamia shughuli za wanafunzi shuleni, kupokea karo, kusimamia mafunzo kwa njia ya posta na mawasiliano ya ana kwa ana.

II. TARATIBU ZA KUANZISHA NA KUSAJILI SHULE.

Ili kuanzisha na kusajili Shule yenye ubora unaostahili wadau hawana budi kufuata hatua mbalimbali kama zilivyoainishwa kwa kina katika **"Mwongozo wa Usajili wa Shule wa Mwaka 1982".** Kwa kifupi hatua hizo ni kama zifutazo:

Hatua ya kwanza: Kibali cha Kujenga Shule

Mwenye nia na uwezo wa kuanzisha Shule atume maombi ya kutaka kujenga shule kwa maandishi kwa Kamishna wa Elimu. Maombi haya yapitishwe kwa Afisa Elimu Wilaya itakapojengwa na Afisa Elimu Mkoa yakiwa na viambatisho vifuatavyo:

- Rejea mwongozo wa andiko la Mradi la Wizara;
- **Bank Statement** yenye zaidi ya **Shilingi Milioni Sitini na Mbili (Tsh. 62,000,000/=**);
- Nakala ya **hati/offer/uthibitisho** wa kumiliki ardhi iliyotolewa kwa matumizi ya Shule inayotambulika kisheria na **Serikali Kuu**, ya **Mtaa na Kijiji** (eneo lisipungue **ekari 7 na nusu** Kijijini na **3 na nusu** Mjini);
- Michoro ya Majengo ya Shule inayoonesha vipimo kwa kuzingatia viwango vya **Wizaya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**;
- Ramani ya Shule inayoonesha mpangilio wa majengo na viwanja vya michezo (Site Plan);
- Cheti cha usajili wa **kampuni/shirika/umoja/NGO** iwapo shule ni ya Jumuiya na **Katiba** yake au **Mkataba wa Maridhiano (Memorandum of understanding or Articles of Association/Partnership deed);**
- Endapo mdau anataka kutumia jina la **Mtakatifu (St.)** awasilishe kibali kutoka kwa **Askofu** wa dhehebu la dini inayotambulika kinachoidhinisha matumizi ya jina hilo.
- Kamishna wa Elimu akiridhika na maombi hayo atatoa kibali cha kujenga Shule kimaandishi, ndipo ujenzi utaanza.

Hatua ya pili: Kuthibitishwa kuwa Mwenye Shule na Meneja wa Shule

Hatua hii ni kwa wale tu waliokamilisha hatua ya kwanza na inahusisha yafuatayo:

- Mwombaji ajaze fomu Na. **RS.6** ya kuomba kuthibitishwa kuwa Mwenye Shule na **RS.7** ya kuomba kuthibitishwa kuwa Meneja wa Shule. Hatua hii itafanywa baada ya mwombaji kuwa amekamilisha ujenzi wa majengo yote muhimu kwa asilimia 75. Majengo hayo ni lazima yawe yamekaguliwa na Mamlaka za Wilaya ambao ni: Mhandisi wa majengo, Afisa Afya na Mkaguzi Mkuu wa Shule wa Wliaya na kwamba fomu hizo ziwe zimepitishwa na Afisa Elimu wa Wilaya, Afisa Elimu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa.
- Wizara ikiridhika itatoa kibali cha maandishi cha kumthibitisha Mwenye Shule na Meneja wa Shule.

Hatua ya Tatu: Maombi ya Kusajili Shule

Hatua hii ni kwa wale tu waliokamilisha hatua ya kwanza na ya pili:

- Mwenye Shule hujaza fomu Na. RS.8 ya maombi ya kusajili Shule baada ya kuwa amekamilisha mahitaji yote yanayotakiwa kwa Shule ya aina anayoiomba ambayo ni: Majengo na samani, vitabu, mihtasari ya masomo na vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuajiri walimu na wafanyakazi wengine wenye sifa na uzoefu.
- Mwenye Shule ambaye Shule yake imetimiza vigezo vyote na Shule kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Shule wa Kanda hupewa taarifa ya kusajiliwa kwa Shule yake kimaandishi. Aidha atapatiwa cheti cha usajili chenye namba ya usajili wa Shule.

Usajili wa Shule za Serikali kuanzia Awali, Msingi na Vituo vya Elimu ya Watu wazima unafanywa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya/Manispaa na Wizara hupatiwa taarifa juu ya usajili wa Shule na Vituo hivyo.

Usajili wa Shule za Kimataifa

Wizara husajili Shule za hadhi ya Kimataifa, usajili huo unafanywa na Taasisi za Kimataifa zinazosajili Shule za aina hii. Wizara huthibitisha na kutambua Shule zinazosajiliwa na taasisi hizo kama za kimataifa. Taasisi hizo ni: European Council for International Schools" (E.C.I.S) na "Association of Internation Schools in Africa" (AISA). Taasisi hizo zimeweka vigezo vya kusajili Shule za Kimataifa. Shule itapewa usajili pale tu itakapotimiza vigezo vyote vilivyowekwa.

Hatua za kufuata ili Shule iwe ya Kimataifa

Mwenye Shule yeyote anayetaka Shule yake iwe na hadhi ya Kimataifa anapaswa kufuata hatua zifuatazo:

- Shule isajiliwe na Wizara kama Shule ya kawaida.
- Mwenye Shule aiombe Wizara kimaandishi kutaka Shule yake iwe ya kimataifa.
- Endapo Wizara itaridhika na ombi hilo itatoa kibali cha maandishi na mwenye Shule ataendelea na hatua za kutuma maombi kwenye taasisi zinazosajili shule hizo.
- Shule itakaposajiliwa kama ya kimataifa, Mwenye Shule aijulishe Wizara kimaandishi na kuambatisha nakala za usajili huo.

Usajili wa Shule/Taasisi za kidini

Taasisi za kidini zinazotaka kuanzisha na kuendesha shule/taasisi za kidini zinapaswa kufuata hatua zote tatu kama zilivyoelezwa isipokua wanapaswa kujaza fomu Na. RS.9 katika hatua ya usajili.

Tanbihi

Uvunjaji wa Sheria kwa namna yoyote ile ni kosa la jinai na adhabu yake ni kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kifungu cha 59.

Ni nani anayehusika na mchakato wa usajili wa Shule?